WAT 0757478868

2026 RATIBA YA KAZI KISWAHILI GREDI YA TANO MUHULA WA TATU

SHULE	GREDI	ENEO LA KUJIFUNZA	MUHULA	MWAKA
	GRADI YA TANO	KISWAHILI	3	

Wiki	Kipindi	Mada	Mada ndogo	Matokeo maalum yanayotarajiwa	Shughuli za ujifunzaji	Maswali dadisi	Nyenzo	Mapendekezo ya tathmini	Maoni
2	1	**Kuandika**	Insha ya maelezo	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a)kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata mtindo na muundo ufaao c) kuchangamkia utunzi mzuri wenye ujumbe mahususi.	Mwanafunzi: -atambue vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi - ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo - aandike insha ya maelezo isiyopungua maneno 150 kwa kuzingatia msamiati unaohusu suala lengwa na kwa kuzingatia vigezo kama vile: ujumbe, tahajia, anwani, muundo, mtindo, mapambo ya lugha k.v methali, nahau, tashbihi, istiari n.k. alizojifunza awali	Je, ni mada gani inayoweza kuandikiwa insha za maelezo?	Vifaa vya kidijitali. vitabu. Chati Mabango Kiswahili Dadisi gredi 5 uk 137-138	Kuandika Kusoma Kutambua vifungu Kujibu maswali Kazi mradi	
	2	**Kusikiliza na kuzungumza**	**Tashbihi:** Tashbihi za tabia	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) Kutaja tabia za viumbe mbalimbali.	Mwanafunzi: -Kutambua tabia za Wanyama mbalimbali k.v. kuongea kama kasuku,mlafi kama fisi. -Kajadiliana kwa vikundi/wakiwa wawili,wawili	Ni tashbihi zipi hutumiwa kuelezea tabia?	Chati. Mabango Vyombo vya kidijitali Kiswahili Dadisi gredi 5	Kujadilia na. Kutunga setensi. Kueleza maana	

				b) Kueleza maana za tashbihi mbalimbali. c) Kufurahia kutumia tabia mbalimbali kuunda sentensi.	maana ya tashbihi k.v. nyeupe kama theluji. -Kuunda sentensi akitumia tashbihi wakiwa pekee yako kwa mfano aliruka kama sungura.		uk 139-140	Kazi mradi	
	3	**Kusikiliza na kuzungumza**	**Tashbihi:** Tashbihi za tabia	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua tashbihi za tabia katika matini b) kutumia tashbihi za tabia kwa usahihi katika sentensi c) kufurahia matumizi ya tashbihi za tabia katika mawasiliano ya kila siku.	Mwanafunzi: -atambue tashbihi za tabia *(k.v. mjanja kama sungura, mlafi kama fisi, mwenye maneno mengi kama kasuku, -eusi kama makaa)* katika vitabu, matini, chati na vyombo vya kidijitali. -aeleze maana ya tashbihi mbalimbali za tabia kwa kutoa mifano -akamilishe tashbihi mbalimbali za tabia akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake darasani -ajaze mapengo katika sentensi kwa kutumia tashbihi mbalimbali za tabia	Ni tashbihi zipi hutumiwa kuelezea tabia?	Chati. Mabango Vyombo vya kidijitali Kiswahili Dadisi gredi 5 uk 139-140	Kujadilia na. Kutunga setensi. Kueleza maana Kazi mradi	
	4	**Kusoma**	**Kusoma Mapana:** Matini ya Kidijitali	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a)kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali b) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma ili kuimarisha umilisi wake wa kutumia tarakilishi . c)Kufurahia kusoma kauli za vifaa vya kidijitali.	Mwanafunzi: -atambue na kuzingatia hatua za kiusalama kutoka kwenye chati au kwenye tarakilishi na mitandao. -atambue jina la faili lengwa kwenye tarakilishi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga -atambue mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake	Unapenda kusoma habari kuhusu nini mtandaoni?	Vifaa vya kidijitali Mabango Chati Kiswahili Dadisi gredi 5 uk 140-141	Kufunga faili Kufungua faili Kusoma kauli.	